

# UINGIZAJI WA VINYAMBUO-NOMINO KATIKA KAMUSI ZA KISWAHILI

*John G. Kiango*

## 1.0 Utangulizi

Wanaleksikografia wa mwanzo wa lugha za Kibantu walikuwa ni wageni kutoka Ulaya na wengi wao walikuwa ni wamishenari k.v. Krapf, L. (1882), Bently, W.H. (1887), Whitehead, J. (1899) na Madan, A.C. (1903), na watumishi wa serikali za kikoloni k.v. Johnson, F. (1939a&b). Kazi zao zinabainisha kuwa tangu awali waliweza kubaini kuwa lugha za Kibantu zina mifumo tata ya kimofolojia. Mifumo hiyo huzalisha maumbo ya maneno ambayo uingizaji wake katika kamusi hutoa changamoto kubwa kinadharia na kwenye njia za kiutendaji.

Mojawapo ya mifumo tata ya kimofolojia katika lugha za Kibantu, ni mfumo wa unyambuaji ambao katika taaluma ya isimu huchukuliwa kama ni mchakato wa kuzalisha maneno mapya unaotumia kanuni za kimofolojia. Mchakato huo huzalisha maneno mapya kwa kupachika viambishi-tamati au viambishi-awali nyambulishi kwenye mizizi ya maneno ya msingi. Maumbo yanayotokana na mchakato huo huitwa vinyambuo. Katika Kiswahili, unyambuaji huzalisha vinyambuo-nomino, vinyambuo-vitenzi, vinyambuo-vivumishi, na vinyambuo-vielezi. Kwa mfano, mzizi **-pend-** unaweza kuzalisha vinyambuo-vitenzi pendea, pendeza, pendeka, pendwa na vinyambuo-nomino upendo, pendo, upendano na mpendwa. Mzizi **-sumbu-** unaweza kuzalisha kinyambuo-vumishi -sumbufu, na mzizi **-nyam-** unaweza kuzalisha kinyambuo-kielezi kinyama. Maneno hayo yanayozalishwa huonekana ni mapya kwa vile hupata fahiwa mpya, ijapokuwa fahiwa hizo zinajiegemeza kwenye maana za msingi za asili za maneno ya msingi. Wakati mwingine, maneno hayo mapya, hupeua maana mpya kabisa ambazo hazihusiani kabisa na maana za asili za maneno ya msingi.

Mchakato wa unyambuaji una tabia kuu nne. Kwanza, unaweza kufanya kinyambuo kuwa na kategoria ya kisarufi ambayo ni tofauti au sawa na ile ya neno la msingi. Kwa mfano kinyambuo *pendwa* [kt] kina kategoria sawa na neno la msingi *penda* [kt], lakini kinyambuo *upendo* [nm] kina kategoria tofauti na neno la msingi *penda* [kt]. Pili, viambishi-nyambulishi huongeza fahiwa mpya juu ya ile inayoelezewa na neno la msingi, mf *penda/pendwa* au kufanya kinyambuo kuwa na maana tofauti kabisa na ile ya neno la msingi mf. *onya/onyesha*. Tatu, kila kanuni ya unyambuaji ina mipaka yake ya kutumika, yaani huwa na uwezo wa kuzalisha maumbo mapya ikitumiwa kwenye maneno fulani ya msingi na hushindwa kufanya hivyo kwenye maneno ya msingi

mengine. Kwa mfano kanuni ya utendwa inayotumia kiambishi-tamati -w-, inaweza kutumika kuzalisha neno jipya *pendwa* kwa kupachika kiambishi hicho kwenye mzizi wa neno la msingi *pend.a*, lakini kanuni hiyo haiwezi kuzalisha neno jipya \**panuwa* kwa kupachika kiambishi-tamati husika kwenye mzizi wa neno la msingi *panu.a*. Hata hivyo kanuni hiyo inaweza kutumika kwenye umbo-tendea la kitenzi hicho yaani *panulia* na kuzalisha kinyambuo *panuliwa*. Nne, kanuni ya unyambuaji ikitumika katika mazingira fulani inaweza kutoa dhana tofauti na ilivyo kawaida. Kwa mfano, kanuni -i- ikitumika kwenye vitenzi mara nyingi huzalisha vinyambuo ambavyo maana yake itakuwa *kitendo kimefanyika kwa niaba ya mtu fulani au kimefanyika mahali fulani au kwa kutumia kitu fulani*. Kwa mfano kitenzi **pika** kinazalisha kinyambuo *pikia* ambacho maana yake ni kuwa tendo la kupika limefanyika mahali fulani, au kwa niaba ya mtu fulani, au kwa kutumia vifaa fulani. Lakini ukitumia kanuni hiyohiyo kwenye kitenzi **pita** ukapata *pitia*, maana zinazoibuliwa sio zile za kawaida tu, yaani za kufanya kwa niaba ya mtu fulani, au kupita mahali fulani, bali unapata maana nyingine kama vile kupita mahali kumwona au kumchukua fulani, kusoma maandishi fulani kwa nia ya kuyaelewa au kuyatathmini, na kwamba ile dhana ya kupita kwa kutumia kifaa fulani haiwezekani kutumika.

Kutokana na tabia hizo nne za mchakato wa unyambuaji, uingizaji wa vinyambuo katika kamusi hutoa changamoto kubwa sana kwa wale wanaosawidi vitomeo vya kamusi na hivyo kulifanya kuwa suala ambalo linatakiwa lishughulikiwe kwa uangalifu.

Yapo maswali ya msingi ambayo mtunga kamusi anapaswa kujiuliza kama vile:

- (i) Je, maana za maneno haya mapya zinaweza kutabirika kwa kujua maana za maumbo ya msingi?
- (ii) Je, maneno haya mapya yaingizwe wapi? Yakae mwishoni mwa kitomeo pamoja na fasili zake au bila fasili?
- (iii) Je, maumbo hayo mapya yanaweza kuingizwa kama vitomeo kamili?
- (iv) Je, ni athari gani zitakazojitokeza kwenye ukubwa wa kamusi kama vinyambuo vyote vilivyozalishwa vitaingizwa vyote kama vitomeo kamili?

Ili kujibu maswali kama hayo, utafiti ujulikanao kama *Uingizaji wa Vinyambuo katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu* ulifanyika mwaka 1992. Utafiti huo umeangalia jinsi vinyambuo-nomino vilivyoingizwa katika kamusi zilizopo na kisha kutoa mapendekezo ya njia bora zaidi ya kushughulikia vinyambuo-nomino. Kwa hiyo, madhumuni ya makala haya ni kuelezea kwa ufupi utafiti huo na matokeo yake.

## 2.0 Mapitio ya kamusi zilizotangulia

Kama tulivyosema kwenye utangulizi, wanaleksikografia wa mwanzo wa lugha za Kibantu waliweza kubaini mifumo tata ya kimofolojia ya lugha za Kibantu walizozindikia kamusi. Kwa hiyo, kila mtunzi wa kamusi alitafuta njia ya kukabiliiana na miundo hiyo tata.

Kwanza, kuna kamusi ambazo zilikwepa kabisa kushughulikia vinyambuo kutokana na utata uliopo wa jinsi ya kuviingiza. Mfano mmojawapo wa kamusi zilizofuata utaratibu huu ni ule wa Hannan (1959) *The Standard Shona Dictionary*. Pili, ziko kamusi ambazo zilikwepa kushughulikia vinyambuo ndani ya kamusi na badala yake zikawa na sehemu ya sarufi na kuitumia sehemu hiyo kutolea ufafanuzi wa masuala ya kisarufi ambayo waliyaona ni magumu kuelezeka au kuyaingiza kwenye kamusi. Mifano ya kamusi zilizofuata njia hii ni ile ya Bentley (1887) *Kikongo-English Dictionary (with Grammar)* na Whitehead (1899) *Bobangi Grammar and Dictionary*.

Tatu, ziko kamusi ambazo zilishughulikia vinyambuo ijapokuwa kwa njia tofauti. Kwa mfano kamusi ya Johnson (1939a) *Swahili-English Dictionary* iliingiza vinyambuo-nomino pamoja na maana zake ndani ya kitomeo cha msingi. Kwa mfano:

**Amua**, v. (1) stop a quarrel, end a dispute, interfere and stop persons quarrelling; (2) judge, be umpire, arbitrate. Prep. **Amulia**, arbitrate between.  
*Tuamulie shauri hili*, decide this case for us.  
Ps. **Amuliwa**, have a case settled by arbitration.  
**Maamuzi**, n. plur. Arbitration, judgement, verdict.  
**Mwamua**, n. wa-, **Mwamuzi**, n. wa- a mediator, arbitrator, umpire, judge. (Cf. *patanisha, suluhisha, hukumu.*) (p.13)

Lakini, kamusi ya Krapf (1882) *Dictionary of Swahili Language*; TUKI, (1981) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* na ile ya Johnson (1939b) *Kamusi ya Kiswahili* zimeingiza vinyambuo-nomino kama vitomeo kamili. Kwa mfano:

**mwamuzi** ji wa- 1. mtu anayetoa hukumu baina ya pande mbili au zaidi zinazohitilafiana; mtu anayesuluhisha ugomvi. 2. mtu mwenye kucheza mchezo fulani na uamuzi wake ndio wa mwisho; refa. (TUKI, 1981 *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*)  
**Mwamuzi** wa- Kama mwamua, lakini hasa hutumika kwa mtu ahukumuye au kukata shauri, jaji, kadhi, hakimu. (Johnson, F. (1939b) *Kamusi ya Kiswahili*)

Kwa upande wa kamusi ya Madan (1903) na ile ya Rechenbach (1968) *Swahili-English Dictionary* imeingiza vinyambuo-nomino kama vitomeo kamili na kuviingiza tena ndani ya kitomeo cha msingi.

Kwa hiyo, mapitio haya mafupi yanaonyesha kwa jinsi gani suala la vinyambuo limewashughulisha watunzi wa kamusi.

### 3.0 Maoni ya wanazuoni kuhusu uingizaji wa vinyambuo

Kama ilivyodokezwa kwenye utangulizi, unyambujaji ni mchakato wa kuunda maneno mapya kutokana na mizizi ya maneno ya aina mbalimbali kwa kutumia kanuni za kimofolojia. Maneno yanayozalishwa hupata maana mpya na wakati mwingine huingia katika kategoria tofauti na neno la msingi.

Kwa muda mrefu sasa, kumekuwepo na mikabala miwili kuhusiana na jinsi ya kuingiza vinyambuo katika kamusi. Mkabala wa kwanza ni wa kutoingiza vinyambuo kwenye kamusi kwa sababu vinaweza kuzalishwa kwa kutumia kanuni za kisintaksia na kimofolojia. (Lyons, 1977:526). Wafuasi wa mkabala huu wanadai kuwa vinyambuo vinaweza vikashughulikiwa vizuri zaidi kwenye vitabu vya sarufi kuliko kwenye kamusi.

Mkabala wa pili ni wa kuingiza vinyambuo kwenye kamusi kama vitomeo kamili kwa kuzingatia hadhi yao kama maneno mapya. Zaidi ya hayo, kanuni za unyambujaji, kwa kawaida hazina uwezo mkubwa wa kuzalisha ukilinganisha na kanuni za uambikaji. Pamoja na hayo, tabia za vinyambuo za kisintaksia na maana zao wakati mwingi hazitabiriki kiurahisi. (Lyons, 1977:524). Kwa hiyo njia bora ya kushughulikia hali kama hizi ni kuviingiza vinyambuo katika kamusi.

Kwa sasa, wanaleksikografia wengi wanaona umuhimu wa kuingiza vinyambuo katika kamusi. Tatizo ambalo bado lipo ni jinsi ya kuviingiza vinyambuo katika kamusi. Inadaiwa kuwa, kwa sababu za kiiktisadi, si jambo jema kuingiza vinyambuo vyote kama vitomeo kamili. Baadhi ya vinyambuo vinaweza kuingizwa ndani ya vitomeo vya maneno ya msingi yaliyozaa vinyambuo hivyo.

Ili kubaini ni vinyambuo vipi vinafaa kuingizwa kama vitomeo kamili na vipi havistahili, wanaleksikografia wamevigawa vinyambuo kwenye makundi mawili; vinyambuo vinavyofuata kanuni na vinyambuo visivyofuata kanuni. Kwa kawaida vinyambuo vyenye kufuata kanuni vinaingizwa ndani ya kitomeo cha neno la msingi kwa sababu maana zake zinatabirika kirahisi. Kwa mfano:

**safisha** *kitenzi* fanya kitu kiwe safi; ondoa uchafu agh.  
kwa maji; futa, pangusa: *Kila mtu anatakiwa kusafisha  
sahani yake baada ya kula. safishia; safishiana; safishika;  
safishiwa; safishwa.*

Kinyume chake, vitomeo visivyofuata kanuni huingizwa kama vitomeo kamili, kwa kuwa maana zake si rahisi kutabirika kutoka kwenye neno la msingi.

**sikiliza** pia **sikiza** *kitenzi* fanya usikie; tega masikio ili usikie kinachosemwa: *Nilisikiliza muziki kwenye radio jana usiku. sikilizana; sikilizia; sikilizika; sikilizwa.*

**sikilizana** pia **sikizana** *kitenzi* elewana, kubaliana au patana katika mambo mabalimbali: *Mimi na marafiki zangu tunasikilizana vizuri.*

Hata hivyo, baadhi ya kamusi zimebainika kukiuka kanuni hii. Katika kamusi hizo, ni jambo la kawaida kuona kinyambuo chenye kufuata kanuni kimeingizwa na kupewa hadhi ya kuwa kitomeo kamili na kile kisichofuata kanuni kimeingizwa ndani ya kitomeo cha neno la msingi (Kiango, J.G. 2000: 117)

#### **4.0 Lengo la Utafiti**

Lengo la utafiti unaohusu Uingizaji wa vinyambuo-nomino katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu lilikuwa:

- i. Kuchanganua uingizaji wa vinyambuo-nomino katika kamusi za Kiswahili kwa lengo la kuboresha uingizaji wake katika kamusi.
- ii. Kuona ni matatizo gani ya kileksikografia yaliyojitokeza katika kutumia njia hizo zilizotajwa.
- iii. Kupendekeza namna ya kuingiza vinyambuo nomino katika Kamusi ya Kiswahili sanifu ambayo haitakuwa na matatizo makubwa.

#### **5.0 Faida za Utafiti**

Utafiti huu unampa fununu mtunga kamusi kuhusu aina mbalimbali za maumbo ya kimofolojia ambayo ni muhimu kuingizwa katika kamusi na njia zinazoweza kutumika katika kuyaingiza. Hata hivyo, uamuzi wa mwisho kuhusu ni maumbo gani ya kuingiza utafanywa na mtunga kamusi mwenyewe kutegemeana na lengo la kamusi na ukubwa wa kamusi inayotungwa.

Utafiti wa maktabani na ule wa uwandani, unaweka bayana taarifa muhimu kama vile ubora na udhaifu wa njia zilizotumiwa katika kuingizia vinyambuo-nomino. Pia kuna taarifa kuhusu kubadilika kwa maana za vinyambuo pamoja na nguvu za kuzalisha za viambishi-tamati nyambulishi vinavyotumika katika kuzalisha

vinyambuo-nomino. Taarifa hizi ni muhimu sana kwa watunga kamusi kwa vile zinasaidia katika kutafuta njia bora za kuingizia vinyambuo-nomino.

### 6.0 Mbinu za Utafiti

Data za utafiti zilikusanywa kutoka maktabani na uwandani. Data za maktabani zilitumika kuchunguza njia zilizotumika kwenye kamusi zilizopo ili kuona ubora na udhaifu wake. Vilevile, data za maktabani zilitumika kuchunguza kubadilikabadilika kwa maana za vinyambuo ili kuona kama maana za vinyambuo zinaweza kubashiriwa kwa kuunganisha maana za viambajengo vyake. Utafiti wa maktabani ulitumia kamusi wahidiya za Kiswahili zifuatazo:

- (a) Frederick Johnson (1939a), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*.
- (b) TUKI (1981), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*.

Vilevile utafiti ulitumia kamusi thaniya za Kiswahili-Kiingereza zifuatazo:

- (a) Ludwig Krapf (1882), *A Dictionary of Swahili Language*.
- (b) Charles Madan (1903), *Swahili-English Dictionary*.
- (c) Frederick Johnson, (1939), *Swahili-English Dictionary*.
- (d) Charles Rechenbach (1968), *Swahili-English Dictionary*.

Katika kuchunguza ubora na udhaifu wa njia zilizotumika, vitenzi sita ambavyo vinawakilisha maeneo mbalimbali ya maana viliteuliwa. Vitenzi hivyo ni: (a) lima (d) vuna (b) zaa (e) cheza (c) pika (f) zika. Data za uwandani zilitumika ili kubaini viambishi vyenye uwezo wa kuzalisha na visivyo na uwezo wa kuzalisha vinavyounda nomino kutoka kwenye vitenzi.

Kuna viambishi vinane (8) ambavyo vinaweza kuambishwa kwenye mizizi ya vitenzi na kuunda vinyambuo-nomino. Viambishi hivyo ni:

- (a) kng-mzt-**ji** mf. m-cheza-ji
- (b) kng-mzt-**o** mf. m-chez-o
- (c) kng-mzt-**zi** mf. m-le-zi
- (d) kng-mzt-**shi** mf. m-pi-shi
- (e) kng-mzt-**i** mf. m-som-i
- (f) kng-mzt-**e** mf. m-tum-e
- (g) kng-mzt-**vu** mf. m-lege-vu
- (h) kng-mzt-**fu** mf. mw-amini-fu

Zingatia kuwa kng maana yake ni kiambishi ngeli, mzt maana yake ni mzizi wa kitenzi na sehemu ya mwisho ndio kiambishi-tamati nyambulishi. Viambishi tamati hivi vilijaribiwa uwezo wake wa kuzalisha kwa kutumia maswali dodoso.

Maswali haya yalitolewa kwa wanafunzi 50 wa sekondari tano za mjini Dar-es-Salaam na walimu wa Kiswahili 17 kutoka katika shule hizo. Zaidi ya hayo, wataalamu wa Kiswahili 21 pia walishiriki: 14 kutoka Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, 3 kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania na 4 kutoka Baraza la Kiswahili la Taifa.

Ili kupima uwezo wa kuzalisha wa hivyo viambishi-tamati nyambulishi nane tulivyoorodhesha hapo juu, ilibidi kuviambika kwenye mizizi ya vile vitenzi sita yaani *-lim-*, *-za-*, *-pik-*, *-vun-*, *-chez-* na *-zik-* na hivyo kuunda mashina ya vinyambuo-nomino 48 yafuatayo:

1. *-limaji*; *-zaaji*, *-pikaji*, *-vunaji*, *-chezaji*, *-zikaji*
2. *-limo*, *-zao*, *-piko*, *vuno*, *chezo*, *ziko*
3. *-limazi*, *-zazi*, *-pikazi*, *-vunazi*, *-chezazi*, *zikazi*
4. *-limashi*, *-zaashi*, *-pikashi*, *-vunashi*, *-chezashi*, *-zikashi*
5. *-limi*, *-zai*, *-piki*, *-vuni*, *-chezi*, *-ziki*
6. *-lime*, *-zae*, *-pike*, *-vune*, *-cheze*, *-zike*
7. *-limavu*, *-zaavu*, *-pikavu*, *-vunavu*, *chezavu*, *zikavu*
8. *-limafu*, *-zaafu*, *-pikafu*, *vunafu*, *-chezafu*, *-zikafu*

Ili kuwa na data inayotosheleza uchambuzi, mashina ya vinyambuo-nomino yaliambikwa viambishi-ngeli vitatu tu ambavyo ni *ki/vi-*; *m/wa-*; na *u/o-*. Muungano huo ulizalisha vinyambuo-nomino 144 na hivyo ndivyo ambavyo yilifanyiwa upimaji. Kwa mfano:

#### **M/WA**

1. **-ji**: *mlimaji*; *mzaaji*; *mpikaji*; *mvunaji*; *mchezaji*; *mzikaji*
2. **-o**: *mlimo*, *mzao*, *mpiko*, *mvuno*, *mchezo*, *mziko*
3. **-zi**: *mlimazi*, *mzazi*, *mpikazi*, *mvunazi*, *mchezazi*, *mzikazi*
4. **-shi**: *mlimashi*, *mzaashi*, *mpikashi*, *mvunashi*, *mchezashi*, *mzikashi*
5. **-i**: *mlimi*, *mzai*, *mpiki*, *mvuni*, *mchezi*, *mziki*
6. **-e**: *mlime*, *mzae*, *mpike*, *mvune*, *mcheze*, *mzike*
7. **-vu**: *mlimavu*, *mzaavu*, *mpikavu*, *mvunavu*, *mchezavu*, *mzikavu*
8. **-fu**: *mlimafu*, *mzaafu*, *mpikafu*, *mvunafu*, *mchezafu*, *mzikafu*

#### **KI/VI**

1. **-ji**: *kilimaji*, *kizaaji*, *kipikaji*, *kivunaji*, *kichezaji*,
2. **-o**: *kilimo*, *kizao*, *kipiko*, *kivuno*, *kichezo*, *kiziko*
3. **-zi**: *kilimazi*, *kizazi*, *kipikazi*, *kivunazi*, *kichezazi*, *kizikazi*
4. **-shi**: *kilimashi*, *kizaashi*, *kipikashi*, *kivunashi*, *kichezashi*, *kizikashi*
5. **-i**: *kilimi*, *kizai*, *kipiki*, *kivuni*, *kichezi*, *kiziki*

6. **-e:** kilime, kizae, kipike, kivune, kicheze, kizike
7. **-vu:** kilimavu, kizaavu, kipikavu, kivunavu, kichezavu, kizikavu
8. **-fu:** kilimafu, kizaafu, kipikafu, kivunafu, kichezafu, kizikafu

#### U/O

1. **-ji:** ulimaji; uzaaji; upikaji; uvunaji; uchezaji
2. **-o:** ulimo, uzao, upiko, uvuno, uchezo, uziko
3. **-zi:** ulimazi, uzazi, upikazi, uvunazi, uchezazi, uzikazi
4. **-shi:** ulimashi, uzaashi, upikashi, uvunashi, uchezashi, uzikashi
5. **-i:** ulimi, uzai, upiki, uvuni, uchezi, uziki
6. **-e:** ulime, uzae, upike, uvune, ucheze, uzike
7. **-vu:** limavu, uzaavu, upikavu, uvunavu, uchezavu, uzikavu
8. **-fu:** ulimafu, uzaafu, upikafu, uvunafu, uchezafu, uzikafu

Watoa habari walitakiwa kuamua iwapo vinyambuo-nomino hivyo vinakubalika au la kwa kuchagua jibu mojawapo kati ya *inawezekana* au *haiwezekani*. Kwa upande wa vinyambuo-nomino ambavyo vingejibiwa *inawezekana*, mtoa habari alitakiwa afanye uamuzi mwingine kwa kuchagua kama ni kinyambuo *'cha kawaida'* katika matumizi au *'sio cha kawaida'* katika matumizi. Kwa kuchagua *'inawezekana'* inamaanisha kuwa kinyambuo hicho kinawezekana kutumika. Kwa kuchagua *'cha kawaida'* humaanisha kuwa ni kinyambuo kinachotumika katika lugha kwa sasa. Kwa kuchagua *'sio cha kawaida'* humaanisha kuwa kinyambuo hicho hakitumiki kwa sasa katika lugha lakini upo uwezekano wa kuweza kukitumia. Kwa upande wa vinyambuo-nomino ambavyo mtoa habari alichagua *haiwezekani* humaanisha kuwa vinyambuo hivyo haviwezi kutumika kama maneno ya kawaida.

## 7.0 Matokeo ya Utafiti

### 7.1 Utafiti wa Maktabani

Data ya maktabani ilionyesha kuwa kuna njia tatu za kileksikografia zilizotumiwa na kamusi sita teule katika kushughulikia vinyambuo-nomino vya vitenzi. Njia hizo ni:

#### 7.1.1 Kitomeo Kamili

Njia hii imetumiwa na Krapf (1882), Johnson (1939a) na TUKI (1981). Vinyambuo-nomino vinaingizwa kama vitomeo kamili. Vinyambuo hivi vinaingizwa kialfabeti kwa kutegemeana na herufi ya kwanza ya kiambishi-ngeli cha umoja. Mfano:

**lima, ku-** Kuchimba ardhi tayari kupanda mbegu ziote.

**Kilimo, vi-** Tendo, maarifa na mavuno ya kilimo, ya kuotesha mavuno.  
**Makulima,** vyombo na kazi ya kulima.  
**Mkulima, wa-** Mlimaji, mtu alimaye.  
**Mlimaji, wa-** Mtu alimaye, mkulima.  
**Mlimo, mi-** Kazi na faida ya kulima; (2) namna ya kulima.  
**Ukulima.** Kazi na mambo yanapopasa kilimo.  
 (Johnson, F. 1939 *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*)

Kwa kutumia njia hii, vinyambuo-nomino haviingizwi ndani ya vitenzi vyao vya msingi. Zaidi ya hayo, chini ya kila kitomeo cha kinyambuo-nomino, hakuna mrejeano unaofanyika kwenda kwenye kitenzi cha msingi.

### 7.1.2 *Si Kitomeo Kamili*

Njia hii imetumiwa na Johnson (1939b) katika kamusi yake ya *Swahili-English* (tofauti na njia ya Kitomeo Kamili aliyoitumia kwenye *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*)

**lima, v.** hoe, cultivate or work land (used of a native mode of cultivation, and nowadays of ploughing also). Ps. **Limwa. St.** and Pot. **Limika,** e.g. be fit for cultivation, arable. Prep. **Limia,** e.g. *jembe la kulimia,* a hoe to dig with. *Nilimlimia shamba,* I cultivated a plantation for him. Cs. **Limisha,** cause to hoe, cultivate, plough, get hoeing done (used of the overseer, *msimamizi*), give permission to begin hoeing (used of the master, Agricultural Officer, rain-makers, &c.).

**Kilimia, n.** the Pleiades (constellation). Prov. *Kilimia kikizama kwa jua huzuka kwa mvua, kikizama kwa mvua huzuka kwa jua,* when the Pleiades set in sun (sunny weather) they rise in rain, when they set in rain they rise in sun. Used of the time to begin cultivating. **Kilimo, n. vi-** (1) hoeing, and so the care of a plantation generally, i.e. cultivation, agriculture; (2) products of cultivation, produce, crops. **-limaji, a.** engaged in agriculture. **Makulima, n.** plur. Implements or operations of agriculture. **Mkulima, n. wa-** (-ku- inserted to dist. From *mlima*) a cultivator, agriculturist, field labourer, peasant, &c. **Mlimaji, n. wa-** same as *mkulima*. **Mlimo, n. mi-** same as *kilimo*. **Ulimaji, n. (ma-)** method (process, fee, &c.) of cultivation, agriculture: and *malimaji,* apparatus, and things used in cultivation. (Johnson, F. 1939 *Swahili-English Dictionary*)

Kwa kutumia njia hii, vinyambuo-nomino vinaingizwa kama vidahizo bila maana zake. Msomaji anaelekezwa kwenda kwenye kitenzi cha msingi kilichozalisha kinyambuo hicho kwa ajili ya kupata maana. Kwa hiyo, kwa njia hii, vinyambuo-nomino hujitokeza tena ndani ya vitenzi vya msingi ambamo maana zao hutolewa. Njia hii humsaidia msomaji kuona uhusiano wa kinyambuo-nomino na kitenzi cha msingi kilichotumika kuzalisha kinyambuo husika. Hata hivyo, upungufu wake ni kwamba njia hii ni ya mzunguko. Ili mtumiaji kamusi aweze kuona kinyambuo-nomino na maana zake kwa haraka, ni lazima aende moja kwa moja kwenye kitenzi cha msingi kilichotumika kuzalisha kinyambuo husika. Sasa kama mtumiaji kamusi hatakuwa na uwezo wa kutambua kitenzi cha msingi, itabidi atumie njia ya kuzunguka. Tatizo hili litawakumba zaidi watumiaji wa kamusi wanaojifunza lugha.

### 7.1.3 *Kitomeo Kamili chenye Mrejeano*

Njia hii imetumiwa na Madan (1903) na Rechenbach (1968). Vinyambuo-nomino vinaingizwa kama vitomeo kamili na kisha kuingizwa tena ndani ya vitenzi vyao vya msingi. Zaidi ya hayo, chini ya kinyambuo-nomino ambacho kimeingizwa kama kitomeo kamili, mrejeano kwenda kwenye kitenzi cha msingi huonyeshwa. Ni rahisi kutafuta kinyambuo kwa njia hii kwa sababu msomaji atakitafuta kialfabeti kama vitomeo kamili vinginevyo. Kwa mfano:

**lima, v. hoe**, the only native mode of cultivation, hence generally 'cultivate, work land' (c.f. mlimo, mkulima, kilimo).

**Mlimaji, n. (wa-)**, for the usual **mkulima**, cultivator, tiller of the ground (cf. lima).

**Mlimo, n. (mi-)** (1) tillage, husbandry, agriculture, cultivation; (2) result of cultivation, i.e. crops, produce (cf. lima, mkulima, kilimo).

**Mkulima, n. (wa-)**, a tiller of the ground, cultivator, agriculturist, field labourer, peasant (cf. lima, mlimaji, and for the form **mkufunzi**, the **ku-** being inserted perhaps to distinguish from mlima, a hill).

**Kilimo, n. (vi-)** (1) hoeing, and so the care of a plantation generally, i.e. cultivation, agriculture; (2) products of cultivation, produce, crops. (cf. lima, mlima, mkulima).

**Makulima, n. plur.** implements or operations of agriculture, tillage (cf. lima, mkulima, kilimo)

**Ukulima, n. (ma-)** condition (employment, operations, etc.) of a husbandman (peasant, tiller of the soil), agriculture, cultivation, peasantry (cf. lima, mkulima, mlimo, kilimo). (Madan, C. 1903 *Swahili-English Dictionary*)

Mbali na waandishi wa kamusi sita zilizofanyiwa uchambuzi kutofautiana katika njia za kushughulikia vinyambuo-nomino, walitofautiana pia katika idadi ya vinyambuo-nomino walivyolingiza kwenye kamusi zao. Krapf (1882) na TUKI (1981) kwa mfano, hawakuorodhesha vinyambuo-nomino vingi katika kamusi zao ukilinganisha na alivyofanya Madan (1903), Rechenbach (1968) na Johnson (1939b). Sababu mojawapo ya kufanya hivyo inawezekana ni kiasi cha ukamilifu ambacho kila mwandishi alijiwekea katika kushughulikia suala hilo. Sababu nyingine zinaweza kuhusiana na ukubwa wa kamusi na kiwango cha kufahamika cha vinyambuo-nomino hivyo.

Ukitafakari njia hizi tatu zilizotumiwa mpaka sasa na kamusi zilizopo, njia inayoelekea kuwa bora ni ile ya kitomeo kamili kwa kuwa kinyambuo-nomino kilichoingizwa kama kitomeo kamili ni rahisi kukitafuta kwenye kamusi. Mabadiliko ya maumbo na uwezo mdogo wa kubaini kitenzi cha msingi kunaweza kumzuia mtumiaji wa kamusi kuona kinyambuo anachotafuta kwa kutumia njia ya si kitomeo kamili.

Sababu nyingine ya kupendelea njia ya kitomeo kamili ni kutokana na ukweli kwamba viko vinyambuo ambavyo vinaweza vikawa na maana nyingi tofauti au maana ambazo hazilingani kabisa na maana za msingi za kitenzi cha msingi. Pili, kinyambuo-nomino kinaweza kuwa na maana ambazo zinahusiana na kitenzi cha msingi lakini ikawa vigumu kutabirika maana hizo kwa kujua tu maana za kitenzi chake cha msingi.

## 7.2 Matokeo ya Utafiti wa Uwandani

Madhumuni mahsusi ya utafiti wa uwandani yalikuwa kupima ni kwa kiasi gani (a) maana za vinyambuo-nomino hufanana au huachana na maana za msingi za vitenzi vilivyozalisha vinyambuo hivyo. (b) viambishi-tamati nyambulishi vina uwezo wa kuzalisha au havina uwezo wa kuzalisha.

### 7.2.1 Maana za Vinyambuo-nomino

Kuhusu maana za vinyambuo, utafiti wa uwandani umegundua kuwa 6.5% ya maana za vinyambuo-nomino vilivyozalishwa kutokana na vitenzi vya msingi, zimekengeuka kabisa. Zaidi ya hayo, utafiti umegundua kuwa 93.5% ya maana za vinyambuo-nomino hivyo vimehifadhi maana za asili za vitenzi vya msingi. Hata hivyo 40.2% ya maana hizo ni maana za kisitari ambazo sio rahisi kuzitabiri. Mfano:

#### (i) Maana zilizokengeuka

**lima**, v. hoe, the only native mode of cultivation, hence generally 'cultivate, work land' (c.f. mlimo, mkilima, kilimo).

**Mlimi, n. (wa-)**, 1. chatterer, gossip, tale bearer 2. boaster, Braggard  
(Madan, C. 1903 *Swahili-English Dictionary*)

(ii) *Maana zinazohusiana na maana ya umbo la msingi*

**lima, v.** hoe, the only native mode of cultivation, hence generally 'cultivate, work land' (c.f. mlimo, mkilima, kilimo).

**Mlimaji, n. (wa-)**, for the usual **mkulima**, cultivator, tiller of the ground  
(cf. lima)

**Mlimo, n. (mi-)** (1) tillage, husbandry, agriculture, cultivation; (2) result of cultivation, i.e. crops, produce (cf. lima, mkulima, kilimo) cultivation, agriculture; (2) products of cultivation, produce, crops. (cf. lima, mlima, mkulima).

**Makulima, n.** plur. implements or operations of agriculture, tillage  
(Madan, C. 1903 *Swahili-English Dictionary*)

(iii) *Maana za kisitiari*

**mzazi** kwa maana ya 'mwanamke aliyejifungua hivi karibuni' **uzazi**  
kwa maana ya 'uwezo wa kuzaa watoto wengi'

Maana hizi haziwezi kutabirika kwa kujua maana ya kitenzi cha msingi **-zaa**.  
(TUKI, 1981 *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*)

**Jedwali 1: Maana za vinyambuo-nomino**

Kitenzi cha msingi	Kudumisha maana ya kitenzi cha msingi	Kukengeusha maana ya kitenzi cha msingi	Jumla ya watafitiwa
Lima	24	0	24
Zaa	31	0	31
Pika	5	2	7
Vuna	10	3	13
Cheza	8	0	8
Zika	9	1	10
<b>Jumla</b>	<b>87 (93.5 %)</b>	<b>6 (6.5 %)</b>	
<b>Kuhifadhi maana za msingi za kitenzi cha msingi</b>			
<b>Zilizohifadhi maana-msingi</b>	<b>52 (59.8 %)</b>		
<b>Zilizopata maana-kisitiari</b>	<b>35 (40.2 %)</b>		

### 7.2.1 Uwezo wa Kuzalisha wa Viambishi-tamati Nyambulishi

Matokeo ya utafiti wa uwandani yaliyotokana na kuwasaili wanafunzi kwa kutumia data ya vitenzi sita ambavyo vinawakilisha maeneo mbalimbali yaani : (a) lima (b) vuna (b) zaa (d) cheza (e) pika (f) zika yamebaini kuwa viambishi-tamati

nyambulishi **-ji** na **-o** vimeonekana kuwa vina uwezo mkubwa wa kuzalisha. Kwa mfano:

#### M/WA

1. **-ji**: mlimaji; mzaaji; mpikaji; mvunaji; mchezaji; mzikaji
2. **-o**: mlimo, mzao, mpiko, mvuno, mchezo, mziko

#### KI/VI

1. **-ji**: kilimaji, kizaaji, kipikaji, kivunaji, kichezaji,
2. **-o**: kilimo, kizao, kipiko, kivuno, kichezo, kiziko

#### U/O

1. **-ji**: ulimaji; uzaaji; upikaji; uvunaji; uchezaji
2. **-o**: \*ulimo, uzao, \*upiko, \*uvuno, \*uchezo, \*uziko

Matokeo hayo yameonyesha kuwa kiambishi-tamati nyambulishi **-ji** kina uwezo mkubwa wa kuzalisha kwa asilimia 86.3 na **-o** kwa asilimia 64.7 kama Jedwali (2) linavyoonyesha hapa chini.

**Jedwali 2: Viambishi-tamati vyenye uwezo mkubwa wa kuzalisha. Majibu ya Wanafuzi**

Shule	Kiambishi-tamati -ji		Kiambishi-tamati -o	
	Inawezekana	Haiwezekani	Inawezekana	Haiwezekani
Azania	58	2	40	20
Tambaza	52	8	36	24
Jangwani	50	10	41	19
Magomeni	50	10	37	23
Kisutu	49	11	40	20
Jumla	259 (86.3 %)	41 (13.7%)	194 (64.7 %)	106 (35.3 %)

Viambishi-tamati nyambulishi vingine, yaani **-zi**, **-shi**, **-i**, **-e**, **-vu**, na **-fu**, vimeonekana havina uwezo mkubwa wa kuzalisha. Maneno machache sana yaliyozalishwa na viambishi-tamati nyambulishi hivyo yamekubaliwa kuwa ni ya Kiswahili. Kwa mfano:

#### M/WA

1. **-zi**: \*mlimazi, mzazi, \*mpikazi, \*mvunazi, \*mchezazi, \*mzikazi
2. **-shi**: \*mlimashi, \*mzaashi, \*mpikashi, \*mvunashi, \*mchezashi, \*mzikashi
3. **-i**: mlimi, \*mzai, \*mpiki, \*mvuni, \*mchezi, \*mziki
4. **-e**: \*mlime, \*mzae, \*mpike, \*mvune, \*mcheze, \*mzike
5. **-vu**: \*mlimavu, \*mzaavu, \*mpikavu, \*mvunavu, \*mchezavu, \*mzikavu
6. **-fu**: \*mlimafu, \*mzaafu, \*mpikafu, \*mvunafu, \*mchezafu, \*mzikafu

## KI/VI

1. **-zi:** \*kilimazi, kizazi, \*kipikazi, \*kivunazi, \*kichezazi, \*kizikazi
2. **-shi:** \*kilimashi, \*kizaashi, \*kipikashi, \*kivunashi, \*kichezashi, \*kizikashi
3. **-i:** kilimi, \*kizai, kipiki, kivuni, kichezi, kiziki
4. **-e:** \*kilime, \*kizae, \*kipike, \*kivune, \*kicheze, \*kizike
5. **-vu:** \*kilimavu, \*kizaavu, \*kipikavu, \*kivunavu, \*kichezavu, \*kizikavu
6. **-fu:** \*kilimafu, \*kizaafu, \*kipikafu, \*kivunafu, \*kichezafu, \*kizikafu

## U/O

1. **-zi:** \*ulimazi, uzazi, \*upikazi, \*uvunazi, \*uchezazi, \*uzikazi
2. **-shi:** \*ulimashi, \*uzaashi, \*upikashi, \*uvunashi, \*uchezashi, \*uzikashi
3. **-i:** ulimi, \*uzai, upiki, uvuni, uchezi, uziki
4. **-e:** \*ulime, \*uzae, \*upike, \*uvune, \*ucheze, \*uzike
5. **-vu:** \*ulimavu, \*uzaavu, \*upikavu, \*uvunavu, \*uchezavu, \*uzikavu
6. **-fu:** \*ulimafu, \*uzaafu, \*upikafu, \*uvunafu, \*uchezafu, \*uzikafu

Baada ya kuchunguza data iliyotokana na vitenzi vyote sita, yaani (a) lima (b) vuna (b) zaa (d) cheza (e) pika, na (f) zika, imebainika kuwa kiambishi-tamati nyambulishi **-zi** kina uwezo mdogo wa kuzalisha kwa asilimia 1.3%; **-shi** 0.7%; **-i** 16.0 %; **-e** 33.3%; **-vu** 3.3% na **-fu** 2 % kama Jedwali (3) linavyoonyesha hapa chini:

### Jedwali 3: Viambishi-tamati visivyo na uwezo mkubwa wa kuzalisha.

#### Majibu ya Wanafunzi:

Shule	K/tamati -zi		K/tamati -shi		K/tamati -i		K/tamati -e		K/tamati -vu		K/tamati -fu	
	Ndio	Sio	Ndio	Sio	Ndio	Sio	Ndio	Sio	Ndio	Sio	Ndio	Sio
Azania	1	59	0	60	2	58	11	49	3	59	0	60
Tambaza	0	60	0	60	13	47	33	27	0	60	0	60
Jangwani	0	60	0	60	4	56	23	37	0	60	0	60
Magomeni	2	58	2	58	20	40	22	38	1	59	6	54
Kisutu	1	59	0	60	9	51	11	49	6	54	0	60
Jumla	4	256	2	298	48	252	100	200	10	290	6	294
	1.3	98.7	0.7	99.3	16.0	84.0	33.3	66.7	3.3	96.7	2.0	98.0
	%	%	%	%	%	%	%	%	%	%	%	%

Uamuzi uliotolewa na walimu na wataalamu wa Kiswahili haukutofautiana sana na ule wa wanafunzi. Wao pia waliona viambishi-tamati nyambulishi vyenye uwezo mkubwa wa kuzalisha ni **-ji** (90.6%) na **-o** (54.9%). Viambishi-tamati nyambulishi visivyo na uwezo mkubwa wa kuzalisha ni **-zi** (16.9%); **-shi** (11.3%); **-i** (26.5%); **-e** (21.8%); **-vu** (10.1%); na **-fu** (11.5 %) kama majedwali (4) na (5) yanavyoonyesha hapa chini:

**Jedwali 4: Viambishi-tamati vyenye uwezo mkubwa wa kuzalisha. Majibu ya Walimu na Wataalamu:**

Asasi	Kiambishi-tamati -ji		Kiambishi-tamati -o	
	Inawezekana	Haiwezekani	Inawezekana	Haiwezekani
Walimu Chuo Kikuu	236	17	144	108
BAKITA	58	14	43	29
Taasisi ya Elimu	51	3	41	13
Walimu Sekondari	512	64	148	158
Jumla	857 (90.6%)	98 (9.4%)	376 (54.9%)	308 (45.0%)

**Jedwali 5: Viambishi-tamati visivyoo na uwezo mkubwa wa kuzalisha. Majibu ya walimu na wataalamu:**

Shule	K/tamati -zi		K/tamati -shi		K/tamati -i		K/tamati -e		K/tamati -vu		K/tamati -fu	
	Ndio	Sio	Ndio	Sio	Ndio	Sio	Ndio	Sio	Ndio	Sio	Ndio	Sio
Walimu Chuo Kikuu	29	223	18	234	84	168	25	227	24	228	33	219
BAKITA	23	49	12	60	22	50	11	61	11	61	12	60
Taasisi ya Elimu	21	33	18	36	23	31	8	46	1	53	4	50
Walimu Sekondari	43	267	29	277	52	254	105	201	33	273	29	277
Jumla	116 16.9 %	568 83.0 %	77 11.3 %	607 88.7 %	181 26.4 %	503 73.5 %	149 21.8 %	535 78.2 %	69 10.1 %	615 89.9 %	78 11.4 %	606 88.6 %

**8.0 Haja ya kuwa na njia mbadala**

Ipo haja ya kuwa na njia mbadala ya kushughulikia vinyambuo-nomino katika kamusi. Kwanza, utafiti wa maktabani umebaini matatizo kadhaa ya kileksikografia yanayotokana na kutumia njia ya "kitomeo kamili", "si kitomeo kamili" na "kitomeo kamili chenye mrejeano."

Tatizo mojawapo ni ule ugumu wa kukipata kinyambuo ndani ya kamusi. Ugumu huu unatokana na kutumia njia ya pili "si kitomeo kamili" ambayo humtaka msomaji awe na uwezo wa kugundua kitenzi cha msingi ndipo aweze kutafuta kinyambuo hicho ndani ya kitenzi cha msingi.

Tatizo la pili ni kushindwa kuonyesha mahusiano kati ya vinyambuo na vitenzi vya msingi. Tatizo hili hujitokeza kwa kutumia njia ya kwanza "kitomeo kamili". Katika njia hii vinyambuo vimeingizwa kama vitomeo kamili tu bila kuonyesha uhusiano wao na vitenzi vya msingi au vinyambuo vingine. Hali hii humnyima mtumiaji mwongozo kamili wa utumiaji.

Tatizo la tatu ni ukosekanaji wa ulinganifu yaani, utumiaji wa kanuni fulani kote katika kamusi. Hali hii imejitokeza kwenye njia ya tatu "kitomeo kamili chenye mrejeano."

Katika njia hii vinyambuo vinaingizwa kama vitomeo kamili, kisha vinaingizwa tena ndani ya vitenzi vya msingi bila maelezo. Zaidi ya hayo chini ya kinyambuo-nomino, mrejeano kwenda kwenye kitenzi cha msingi huonyeshwa. Mwisho, kinyambuo hurejeshwa kwenye vinyambuo vinavyohusiana kimaana na kwenye vile vinavyoshirikiana vitenzi vya msingi. Tatizo lililojitokeza katika baadhi ya kamusi zilizotumia njia hii ni kule kufanya mrejeano ambao hauna ulinganifu. Baadhi ya vinyambuo katika baadhi ya kamusi hizo vimerejeshwa ama kwenye vinyambuo ambavyo vinahusiana kimaana tu na vingine kwenye vinyambuo vinavyoshirikiana kitenzi cha msingi tu na wala sio kote kuwili. Ingekuwa jambo bora kama utaratibu mmoja ungeteuliwa na kutumika katika vinyambuo vyote ili kuwe na ulinganifu.

### **9.0 Pendekezo la Njia Mbadala**

Njia mbadala inayopendekezwa itumike katika kushughulikia vinyambuo-nomino kwenye kamusi za Kiswahili ni ile ya "kitomeo kamili chenye mrejeano wenye ulinganifu". Inapendekezwa vinyambuo-nomino viwe vitomeo kamili kwa sababu kuu mbili: kwanza, utafiti umebaini kuwa vinyambuo-nomino vinavyotokana na vitenzi sio mara zote fahiwa zake zinaeleweka kiurahisi kwa kuzijua tu maana za asili za vitenzi vya msingi. Kadhalika kuna vinyambuo vyenye maana za kisitari ambazo sio rahisi kuzifahamu kwa kujua tu maana za vitenzi vya msingi. Zaidi ya hayo, viko vinyambuo ambavyo huchukua maana ambazo hazihusiani hata kidogo na maana za asili za kitenzi cha msingi. Kwa hali hii, inapendekezwa kuwa ni vema vinyambuo-nomino vikaingizwa kama vitomeo kamili.

Jambo la pili ni kwamba njia hii inapendekezwa kwa vile idadi ya vinyambuo vinavyoweza kuzalishwa na viambishi-tamati nyambulishi sio vingi sana kiasi cha kutishia kuchukua nafasi kubwa katika kamusi. Kama ilivyoelezwa awali, utafiti huu umebaini kuwa ijapokuwa kuna viambishi-tamati nyambulishi nane vinavyotumika katika kuzalisha vinyambuo-nomino, ni viambishi-tamati viwili tu ambavyo vina uwezo mkubwa wa kuzalisha na sita havina uwezo mkubwa wa kuzalisha. Kwa hiyo vinyambuo-nomino vitakavyozalishwa havitakuwa vingi sana na hivyo kamusi zinaweza kuviingiza vyote kama vitomeo kamili.

Tatu, njia hii inapendekezwa iwe pia na mrejeano. Imebainika kuwa mrejeano unampa mtumiaji kamusi mwongozo kamili wa matumizi ya vinyambuo-nomino. Mrejeano unaopendekezwa ni ule wa kuorodhesha tena vinyambuo-nomino vyote ndani ya vitenzi vya msingi. Pili, kinyambuo-nomino kikishaingizwa kama kitomeo kamili kifanyiwe mrejeo kwenda kwenye kitenzi chake cha msingi, na

kwenye vinyambuo-nomino vinavyohusiana kifahiwa tu. Na mwisho ili kupata ulinganifu, utaratibu huu ufuatwe kwa vinyambuo-nomino vyote. Kwa mfano:

**lima** *kt* andaa shamba liwe tayari kwa kupandwa mbegu; safisha na tifuu udongo ili uweze kupanda mbegu. **kilimo** *nm.* **mkulima** *nm.* **mlimaji** *nm.* **mlimo** *nm.* **ukulima** *nm.* **ulimaji** *nm.*

**kilimo** *ji* shughuli za ukulima. **lima** *kt.* **mlimaji** *nm.* **mlimo** *nm.* **ukulima** *nm.* **ulimaji** *nm.*

**mkulima** *ji* (wa-) 1 mtu anayepata mahitaji yake kutokana na jasho lake kwa kulima ardhi. 2 mtu mwenye ujuzi na maarifa na ustadi wa kulima. **lima** *kt.* **kilimo** *nm.* **mlimaji** *nm.* **mlimo** *nm.* **ukulima** *nm.* **ulimaji** *nm.*

**mlimaji** *ji* (wa-) mtu mwenye ujuzi wa kulima ambaye agh. huajiriwa ili kufanya kazi hiyo. **lima** *kt.* **kilimo** *nm.* **mlimo** *nm.* **ukulima** *nm.* **ulimaji** *nm.*

**mlimo** *ji* mtindo wa kusafisha na kupanda mazao. **lima** *kt.* **kilimo** *nm.* **mlimaji** *nm.* **ukulima** *nm.* **ulimaji** *nm.*

### Zingatia

Ili kumsaidia mtumiaji asidhani kuwa vinyambuo vilivyoingizwa ni visawe vya kidahizo msingi, vinyambuo hivyo lazima viwe kwenye chapa iliyokoza na vionyeshwe kategoria yake mwishoni.

### 10.0 Hitimisho

Makala haya yamechambua njia zilizotumiwa na kamusi zilizopo za Kiswahili, wahidia na thaniya, katika kushughulikia vinyambuo-nomino. Data kutoka maktabani imesaidia kuonyesha ubora na udhaifu wa njia hizo na data kutoka uwandani imetupa picha kuhusu kiasi cha uwezo wa kuzalisha uliomo ndani ya viambishi-tamati nyambulishi vinavyotumiwa kuambishwa kwenye maumbo ya msingi ya vitenzi.

Uchambuzi wa data za maktabani na matokeo ya data kutoka uwandani yamesaidia katika kutoa pendekezo la njia bora ya kutumia katika kushughulikia vinyambuo-nomino vya vitenzi.

## MAREJEO

Bentley, William Holman. (1887) *Kikongo-English Dictionary* (with Grammar). London: Baptist Missionary Society.

Bauer, Laurie. (1983). *English Word-formation*. Cambridge: Cambridge University Press.

- Hannan, M. (1959) *The Standard Shona Dictionary*. Jesuit Missionary Society. IKR. 1981. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- Johnson, F. (1939a). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- (1939b) *Swahili-English Dictionary*. Nairobi: Oxford University Press.
- Kiango, J.G. (1992) *Swahili Dictionary Design*. Ed.D Dissertation. Columbia University, USA.
- Kiango, J.G. (2000) *Bantu Lexicography: A Critical Survey of the Principles and Process of Constructing Dictionary Entries*. Tokyo: ILCAA.
- Krapf, L. (1882) *A Dictionary of the Swahili Language*. London: Trubner & Co.
- Lyons, John *Semantics 2* Cambridge, New York. Cambridge University Press.
- Madan, A.C. (1903) *Swahili-English Dictionary*. London: Oxford at the Clarendon Press.
- Rechenbach, C. (1968) *Swahili-English Dictionary*. New York: Catholic University of American Press, INC.
- Whitehead, John. (1899) *Bobangi Grammar and Dictionary*. London: Baptist Missionary Society.